JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Shule ya Sekondari Missungwi,
S. L. P. 62
MISUNGWI.
Tarehe……

Namba za Simu:

Mkuu wa Shule: 0783 – 882020
Makamu Mkuu wa Shule: 0756 – 543983
Matron: 0768 – 467298

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
……
S. L. P……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MISSUNGWI KIDATO CHA TANO ILIYOKO HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI MKOA WA MWANZA MWAKA 2018/2019.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…… tahasusi ya…… Shule ya Sekondari Missungwi ipo umbali wa kilometa 1.5 kutoka Makao Makuu ya Halmshauri upande wa Mashariki.

   Kwa wanafunzi wanaotokea Mikoa ya KAGERA, KIGOMA, GEITA, MWANZA na MARA shuka stendi kuu ya mabasi ya NYEGEZI, panda HIACE zinazoelekea Buhongwa ambapo kuna kituo kikuu cha HIACE zinazokuja Misungwi; omba wakushuhe ubao wa sekondari Missungwi, nauli ni Tsh.1,500/=. Na wale watakaosafiri na barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, shuka stendi ya Misungwi na panda usafiri wa pikipiki hadi shuleni kwa gharama ya Tsh.1,000/=

   Muhula wa masomo unaanza tarehe……. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……. mwisho wa kuripoti ni tarehe…….

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 Sare za Shule.

(ii) Sketi mbili ndefu za Blue sky mshono wa rinda box.

NB: Kitambaa kiwe kizito cha suti na sketi ifike kwenye kifundo cha mguu (zingatia).

(iii) Shati mbili nyeupe mikono mirefu.

(iv) Hijabu nyeupe kwa waislam.

(v) Jezi ya michezo rangi nyeupe.

(vi) Viatu nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi pair mbili.

(vii) Raba nyeupe ya michezo.

(viii) Nguo ya kushindia (shamba dress) rangi ya pink gauni ivuke magoti na iwe na mikono ya shati mifupi na suruali yake rangi ya pinki isiyobana mwili (Modo hazitakiwi).

(ix) Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.

(x) Sweta rangi ya dark blue.

NB: kama kuna utata juu ya ushonaji wa sare na nguo za kushindia njoo ushonee shuleni.

2.2 Ada na michango ya shule.

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi Tsh.70,000/= unaweza kulipa kiasi cha Tsh.35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kupitia kwenye akaunti ya shule **E.K. Account ni E.K Missungwi Secondary School Account Na 31310002628 NMB.**

na uje na PAY IN SLIP (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip).

(b) Michango.

(i) Ukarabati wa samani Tsh.15,000/= ilipwe E.K Account.
(ii) Taaluma Tsh.20,000/= ilipwe E.K Account.
(iii) Walinzi na wapishi Tsh.30,000/= ilipwe E.K Account
(iv) Tahadhari Tsh.5,000/= (hairejeshwi). E.K Account.
(v) Huduma ya kwanza Tsh.10,000/=. E.K Account.
(vi) Nembo Tsh.2,000/= kwa kila nembo (nembo 2). E.K Account.
(vii) Kitambulisho na picha Tsh.6,000/= E.K Account.
(viii) Mtihani wa kujipima Tsh.20,000/= E.K Account.

E.K. Account ni E.K Missungwi Secondary School Account Na 31310002628 NMB.

(c) Vifaa vya Shule.

(i) Rimu ya karatasi 1 A4 kwa mwaka.
(ii) Folder file moja.
(iii) Kwanja, mfagio wa nje (chelewa)na mfagio wa ndani(soft broom) EGM & HGK
(iv) Jembe 1lenye mpini na reki moja yenye mpini CBG & HGL

(d) Mahitaji ya mwanafunzi.

(i) Vitabu vya masomo ya tahasusi yake (vitakaguliwa)
(ii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.
(iii) Scientific calculator kwa CBG na EGM.
(iv) Godoro futi tatu na nusu kwa sita. Tafadhali zingatia vipimo.
(v) Mashuka pair 2 rangi ya blue, foronya 1 na chandarua 1 pembe nne (4 x 6ft) nyeupe, blanketi 1.
(vi) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
(vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko (lita 10).
(viii) Tranka (sanduku la bati).
(ix) Taulo ya kuogea.
(x) Taulo special za kike.
(xi) Ndala.
(xii) Khanga doti moja.
(xiii) Nguo za kulalia usiku.
(xiv) Nguo za ndani za kutosha, toilet paper, sabuni za kuogea na kufulia, dawa ya meno na mswaki, mafuta ya kupaka n.k.
(xv) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa/Affidavit
(xvi) Result slip (Hati ya matokeo).

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**
   (i) Wizi.
   (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
   (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
   (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
   (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
   (vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
   (vii) Kufuga ndevu.
   (viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
   (ix) Uvutaji wa sigara.
   (x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
   (xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
   (xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
   (xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
   (xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
   (xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
   (xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
   (xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu.**
   a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
   b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
   c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   d) Picha (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule……

Jina la Mkuu wa Shule……**...**

Mhuri wa Mkuu wa Shule…….

ORODHA YA VITABU VYA KUJA NAVYO

1. ECONOMICS:

- Economics for Advanced Level paper and professional studies. By AMBILIKILE.
- Economics for Advanced Level Paper two and Professional studies. By AMBILIKILE.

2. GEOGRAPHY:

- Practical Geography Alive Advanced Level By ZIST KAMLI January 2016.
- Geography Review Advanced Level paper 1 & paper 2.

3. ADVANCED MATHEMATICS:

- Pure Mathematics 1&2 by J.K. BACKHOCES S.P.T Houldworth revised by P.J.F HORRIL NEW EDITION
- Tranter C.J Advanced Level Mathematics
- Chand S. Mathematics for Advanced Level Class XI and XII

4. BAM:

- BASIC AND APPLIED MATHEMATICS (BAM) FOR ADVANCED LEVEL BY RESPICIUS KIIZA & LUGANO MWANGINDE

5. BIOLOGY:

- BIOLOGICAL SCIENCE
- UNDERSTANDING BIOLOGY
- CHANDY CLASS XI, CLASS XII

6. CHEMISTRY:

- ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY PART ONE AND TWO BY TIE(1995)
- ADVANCED LEVEL PHYSICAL CHEMISTRY WITH GENERAL CHEMISTRY BY AFICAN PROPER EDUCATION NETWORK (APE).. FIRST EDITION 2011SECOND EDITION 2012
- ORGANIC CHEMISTRY PART ONE AND TWO …MZUMBE PROJECT AU TIE.
- ORGANIC CHEMISTRY. BY SOLOMON AND CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI BY DK. S.K JAIN (CHANDY).

NB: Nunua vitabu kulingana na Tahasusi yako.

FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE

Mimi Mzazi/Mlezi wa…… nimesoma kwa makini kanuni, sheria, maagizo ya shule na kuyaelewa vema. Endapo kijana wangu ataenda kinyume na kanuni, sheria na maagizo hayo, achukuliwe hatua sitahiki.

Jina……..

Saini..…….

Tarehe……..

PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI/NDUGU WA MWANAFUNZI……..……

KIDATO CHA……..... MWAKA……..…

Anuani ya Mzazi/Mlezi/Ndugu

1. Jina……
   Anuani ……
   Uhusiano……..
   Simu……

Picha

2. Jina……
   Anuani ……
   Uhusiano……..
   Simu……

Picha

3. Jina……
   Anuani ……
   Uhusiano……..
   Simu……

Picha

4. Jina……
   Anuani ……
   Uhusiano……..
   Simu……

Picha

Jina la Mzazi/Mlezi/Ndugu

……

Sahihi……

Tarehe……..

HISTORIA FUPI YA MWANAFUNZI.

I. Jina la Mwanafunzi…….

Tarehe ya kuzaliwa……

Mahali alipozaliwa……..

Shule ya Msingi……

Shule ya Sekondari……

Dhehebu analosali……..

II. Jina la Mzazi/Mlezi……

Mahali anapoishi……

Kata…….Wilaya……. Mkoa…….

Kazi…….

III. Hali ya Afya yake

- **Magonjwa Sugu**
  1. ……
  2. ……
  3. ……

IV. Habari nyinginezo

……

……

……

Jina la Mzazi…….

Saini……..

Tarehe……..